**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**KUMB.NA: ILLGSS/FI/2026** **Tarehe: 01/12/2025**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………….…………..**
…………………………………………………………….…...
…………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO**

**………………………………………………………………………………**
**KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILULU.**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika **Shule ya Sekondari Ilulu.**

Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake. **Shule ya Sekondari Ilulu** ipo **Mkoa wa Lindi Wilaya ya Kilwa kijiji cha Njianne. Shule ipo umbali wa mita 500 kutoka kituo cha basi cha kijiji cha njianne. Unaweza kufika shuleni kutokea Dar es salaam kwa usafiri unaopatikana kituo cha mabasi cha mbezi au mbagala rangitatu na USHUSHWE KIJIJI CHA NJIANNE. Kwa wanaotokea njia ya kusini yaani LINDI, MTWARA NA RUVUMA UNATAKIWA USHUSHWE PIA KWENYE KIJIJI CHA NJIANNE. KARIBU SANA**

Kutoka kituo cha basi cha njianne hadi shuleni nauli ya bodaboda ni shilingi elfu moja( Tsh 1000/=) tu.
UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI TAREHE /01/2026.

Pamoja na barua hii, pokea,

(a) Fomu ya kupimwa afya ya mwanao. Apimwe kwenye Hospitali ya Serikali. Hakikisha anapimwa sio kujaziwa fomu tu, na umwelekeze Mganga matatizo ya kiafya aliyonayo mwanao,kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya daktari.
(b) Fomu ya kuonyesha ndugu wa karibu na ikiwa na anuani, namba za simu na sehemu anakoishi pamoja na
ahadi ya kutekeleza wajibu.

Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema ya mwanao kuja kujiunga nasi. (MOTTO “ ELIMU KWA MAENDELEO”).

**KARIBU ILULU SEKONDARI**

…………………......

AMINA S. MANDALI

MKUU WA SHULE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
## SARE ZA SHULE:

1. **Sketi ya shule**

- ❖ Mwanafunzi anatakiwa aje na sketi ndefu ya shule rangi ya damu ya mzee (maruni) ambayo kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi isizidi sentimita 18 au nchi saba na nusu yenye mshono wa linda box au anaweza kuja kushona shuleni kwa gharama ya kiasi cha t-shs 27,000/=tu kwa sketi moja.
- ❖ Mwanafunzi anashauriwa awe na sketi mbili (02) au zaidi.

2. **Shati /nusu kanzu ya shule**

(i) Shati nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mifupi tetroni – Tomato
(ii) Kwa wanafunzi wa Kiislamu.
- Nusu kanzu nyeupe na sio shati la mkono mirefu.
- Hijabu nyeupe (kitambaa cha harua) na sio mtandio wala juba, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

AIDHA mwanafunzi aje na
(iii) Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi
(iv) Viatu vyeusi vyenye gidamu (kamba) (**VISIWE NA VISIGINO VIREFU**) jozi mbili (02).
(v) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.
(vi) Track Suit nyeusi yenye ufito mweupe na t-shirt nyeusi isiyobana na isiyokuwa na maandishi yoyote (raundi kola) kwa ajili ya michezo na maandalizi ya jioni.

3. **Gauni la kazi za nje**

Mwanafunzi anatakiwa aje na gauni la kazi za nje la kitambaa kizito (shamba dress) rangi ya **Kijani ya bendera ya taifa,** mshono wa solo la kuunga, kama anavaa hijabu ashone ya rangi **ya Kijani** AU anaweza kuja kushona gauni shuleni kwa gharama ya t-shs 35,000/ kwa wasiovaa hijabu na gharama ya t-shs 43,000/= kwa wanaovaa hijabu (yaani gauni na hijabu).Wanafunzi watavaa gauni ya kijani muda wote watapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo.

4. **T-shirt na sweta la shule**

Mwanafunzi anatakiwa awe na t-shirt ya rangi ya njano yenye nembo ya shule ambayo inapatikana shuleni kwa kiasi cha shilingi elfu kumi na nne (14,000/=) tu, na sweta la rangi ya damu ya mzee yenye nembo ya shule ambayo pia inapatikana shuleni kwa kiasi cha shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) tu.Wanafunzi watavaa t-shirt kila siku ya jumatano na sweta watavaa kipindi chote cha baridi.

5. **Nguo nyingine**

-Aje na nguo za ndani, khanga/ kitenge doti mbili pamoja na nguo ya kulalia (Night dress).
-Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine za nyumbani nje ya zilizotajwa hapo juu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**NB:**

- Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule kama atakuwa ameshona nyumbani siku ya kuripoti na kama hajashona aje akiwa amevaa track suit iliyoagizwa.

- Mwanafunzi anatakiwa kuvaaTrack Suit wakati wa maandalio ya jioni ili kujizuia na mbu.
- Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule.
- Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni au nje ya shule.

## MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA MWANAFUNZI

Mwanafunzi anatakiwa;

(i) Awe na sanduku (nunua sanduku la bati zito) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.
(ii) Awe na Godoro moja la futi 2.5(mbili na nusu) ambalo linapatikana shuleni kwa tshs elfu 45,000/= tu kwa matumizi yake binafsi (pesa ya godoro uje nayo mkononi).
(iii) Alete chandarua nyeupe/pinki ya kitanda cha futi 2.5(futi mbili na nusu).
(iv) Aje na Mto na Foronya yake ya pinki kwa anayetumia.
(v) Aje na Shuka za kulalia mbili za futi 2.5 (rangi ya pinki isiwe na maua) nayo inapatikana shuleni kwa kiasi cha shilingi 18,000/= kwa zote mbili.
(vi) Aje na vifaa vya usafi binafsi kama mswaki, sabuni n.k
(vii) Aje na ndoo ndogo 2 nazo zinapatikana shuleni kwa bei ya shilingi 10,000/= kwa zote mbili.
(viii) Aje na taulo moja.
(ix) Aje na kandambili kwa ajili ya kuogea.
(x) Aje na viatu vya kushindia rangi yoyote (viwe vya wazi).
(xi) Aje na bakuli lenye sehemu nne liwe na mfuniko, kikombe na kijiko (vyombovya chakula).
(xii) Aje na madaftari makubwa kumi (10).
(xiii) Aje na Mathematical set moja (1) kwa matumizi yake awapo darasani.
(xiv) Aje na vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yake.
(xv) Aje na Bima ya afya kama anatumia bima inayotokana na mzazi au mlezi wake ili kurahisisha matibabu.**KAMA HANA HAKIKISHA MZAZI/ MLEZI UNAKUJA NA KIASI CHA TSH 52,000/= KWA AJILI YA KUMKATIA BIMA YA AFYA YA NHIF SHULENI. BIMA YA AFYA NI MUHIMU SANA.**

## MAAGIZO MUHIMU YA SHULE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**


**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com


i. Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi

- fyekeo(slasher) moja lililonolewa
- Sabuni ya chooni ya maji lita tano (lita 5)
- Fagio la chelewa la kusimama (la wima) moja kwa kila muhula

NB: Vifaa vyote vinapatikana karibu na eneo la shule

PIA

ii. Alete nakala ya cheti cha kuzaliwa.
iii. Aje na rimu moja isiyokuwa na mistari (nyeupe A4)
iv. Aje na picha za passport mbili alizovaa shati la shule zilizopigwa hivi karibuni.

**CHAKULA**

Shule hutoa chakula ambacho huliwa na watanzania wote ambacho serikali inapendekeza kuliwa na wanafunzi. Endapo mwanafunzi ana miiko ya kutokula vyakula fulani, tafadhali usipokee nafasi hii kwani shule haitatoa huduma pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo usilete chakula kama mchele, unga, biskuti, mkate, kinywaji cha aina yoyote n.k nahaturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/ kinywaji toka nje ya shule.

**FEDHA ZA MATUMIZI**

Mwanafunzi afunguliwe akaunti, benki ya **NMB/CRDB** kwa ajili ya kumtumia pesa za matumizi binafsi.Kwa mwanafunzi asiye kuwa na akaunti ya NMB/CRDB atawasiliana na mzazi kuhusu kutumiwa pesa ya matumizi kwa mwalimu wa darasa kwa njia ya meseji . Aidha mzazi anaweza kuwasiliana na mwalimu na kutuma pesa ya matumizi ya mtoto wake siku yoyote bila kuwasiliana na mwanafunzi.

**TAARIFA YA UGONJWA KWA MWANAFUNZI**

Taarifa yoyote ya ugonjwa wa mwanafunzi utapewa na makamu mkuu wa shule au matroni wa shule kwa maelekezo ya mkuu wa shule. Usipokee taarifa yoyote inayomuhusu mwanafunzi kutoka kwenye chanzo chochote kingine.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

## ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

i. Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

**ii.** Mawasiliano yoyote yanayohusu taarifa ya msiba,ugonjwa wa wazazi,walezi au ndugu yeyote wa mwanafunzi , yafanyike kupitia **mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule au ofisi ya malezi . Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni.**

iii. Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.

iv. Mzazi/mlezi unashauriwa kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivuwa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.

v. **Hakutakuwa na siku za kuwatembelea wanafunzi.**Wanafunzi wataendelea kutumia likizo za serikali kama mihula itavyoelekeza.

vi. Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofungwa. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufungwa.

vii. Mzazi/mlezi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.

viii. Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa mkuu wa shule. Hii itarahisisha kwa muuguzi au ‘matroni’ kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, atapokelewa tu, kupata elimu ni haki yake.

ix. Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

x. Shule itakapofungwa, likizo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi/mlezi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofunguliwa atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi/mlezi) moja kwa moja kuja shuleni. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.

**xi.** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. **Akija navyo atafukuzwa shule (atafutwa masomo mara moja).**

**N.B: Tafadhari mshauri mwanao azingatie/afuate maelekezo yote aliyopewa! Akipatikana nakosa litakalomsababishia arudishwe nyumbani, atajigharamia nauli ya kwenda na kurudi.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

## SHERIA ZA SHULE

a) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote.
b) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k.
c) Yapasa kuweka shule, eneo lako na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote.
d) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa
e) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani wakati wa kujisomea.
f) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake.
g) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, earphones'' pamoja na redio.
h) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka utoaji wa taarifa zisizo sahihi na rasmi kwa wazazi/walezi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia ofisi ya makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi tu.
i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani
j) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu/jamaa yake aendapo msikitini, kanisani au hospitalini bila ya ruhusa kutoka shuleni. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na uongozi wa shule.
k) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.
l) Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl, nywele za bandia, mapambo kama bangili, heleni, mikufu n.k. havitakiwi kabisa shuleni.
m) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa.
n) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa,Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani (kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi).
o) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika ofisi ya matroni).
p) Mwanafunzi **haruhusiwi kusuka nywele**, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni, urefu unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana. Haruhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k.
q) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo shuleni.
r) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika katika eneo la mabweni.
s) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa kwa kusalimiana tu.
t) Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shule ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

u) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule. Hakuna ruhusa yoyote itakayotolewa mapema kabla ya siku rasmi ya kufunga shule.
v) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la kinidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba, shangazi, kaka n.k.
w) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupigana na mtumishi au mwanafunzi mwenzake.
x) Mwanafunzi haruhusiwi kutukana au kutumia lugha chafu kwa mtumishi au mwanafunzi mwenzake.
y) Mwanafunzi haruhusiwi kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya mtu mwingine.
z) Mwanafunzi haruhusiwi kuanzisha, kushawishi na kushiriki mgomo.

**Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo kwa muda (suspension) iwapo atakiuka sheria za shule**.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA ..........**

**Mimi** ………………………………………………………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ilulu. **NIMEKUBALI/NIMEKATAA (kata isiyo husika)** nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilulu. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

**Jina la mwanafunzi** ……………………………………..……… **Sahihi** …….……….… **Tarehe** ……….

**Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………………..……… Sahihi ……………..….Tarehe ……………**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139. **KILWA.**
ilulugss@gmail.com




**MFANO WA MSHONO WA SKETI YA SHULE**




**MFANO WA MSHONO WA SHAMBA DRESS**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**FOMU NAMBA 1.**

**To the Medical Officer**
……………………………………………………………………….…
……………………………………………………………………….**.**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO …….…………………………………………**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood…………………………………………………………………………………...
2. Stool ………………………………………………………………………………...
3. T.B. Test ……………………………………………………………………………….
4. Syphilis Test …………………………………………………………………………...
5. Urine Examination …………………………………………………………………….
6. Eye Test ……………………………………………………………………………….
7. Chest Test ……………………………………………………………………………...
8. Ears Test ……………………………………………………………………………….
9. Spleen ………………………………………………………………………………….
10. Abdomen ………………………………………………………………………………
11. Pregnancy………………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
I certify that, the above pupil is suitable/ unsuitable for secondary school students. If unsuitable givereasons:
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

Name of **Medical Officer**: …………………………………………… Signature ………………………
Date: ……………………………………… Official stamp ……………….............

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Mkoa …………………..……………………… Wilaya …………………………………………
2. Tarafa ……………………………………………. Kata …………………………………………
3. Mtaa/Kijiji ……………………………………………
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………..………….Saini………………….
   Tarehe………………………………. Mhuri……………………………. Simu…………………...
5. Michezo anayopendelea

| Na. | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

9. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na. | Aina ya Uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

**NB**: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na cheti chako cha kuzaliwa.

**Jina la Mwanafunzi ……………………………………..Saini ………………… Tarehe ……………**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0782586468/0717402768
0682825963/0684971079

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, **KILWA.**
ilulugss@gmail.com

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………….
2. Kazi …………….…………………………………………………………………………………...
3. Anuani …………………………………………… Namba ya simu ……………………………….
4. Mkoa ………………………… Wilaya ……………………….. Tarafa …………..……………….
5. Kata ………………………………………Mtaa/Kijiji …………………………………………….
6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

Mimi Mzazi/Mlezi wa..............................................................................................ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Ilulu katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

**Jina la Mzazi/Mlezi …………………………………Saini............................ Tarehe………............**